Toleo Na.06 // | Julai, 2020 www.habari.go.tz

# JARIDA

## WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO



# Maoni ya Mhariri

Usiku wa kuamkia Julai 24, 2020 Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, Dkt.John Pombe Magufuli akiwa Ikulu Chamwino Jijini Dodoma alilitangazia Taifa kuhusu kifo cha Rais wa Awamu ya Tatu, Mzee Benjamin William Mkapa aliyefariki hospitalini Jijini Dar es Salaam.

Hakika Taifa limempoteza mwanadiplomasia nguli aliyewahi kutokea Afrika na duniani, ambaye atakumbukwa kwa kusuluhisha migogoro mbalimbali ya kisiasa katika nchi za Kenya na Burundi pamoja na mchango wake katika kuhimiza na kulinda amani barani Afrika.
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo itamkumbuka kwa mchango wake alipohudumu kwa nafasi ya Waziri wa Habari na Utangazaji mwaka 1990 hadi 1992, na alipokuwa Mhariri wa The Nationalist (Baadae Daily News) na Mtendaji Mkuu wa Shirika la Habari Tanzania (SHIHATA) mwaka 1974
.

Aidha, Mzee Mkapa alikuwa mwanahabari mkongwe na kiongozi aliyeleta mabadiliko makubwa katika kuiendeleza tasnia ya habari na michezo katika kipindi chake cha uongozi.
Wakati wa uhai wake akiwa Rais wa Awamu ya Tatu alianzisha Vitengo vya Habari na Mawasiliano Serikalini ambao ndiyo wasimamizi wa masuala ya habari serikalini. Kwa upande wa tasnia ya michezo alijenga Uwanja wa Michezo wa Kimataifa jijini Dar es Salaam ujulikanao kama Uwanja wa Taifa.

Buriani Baba Yetu Benjamin Wiliam Mkapa, Tutakukumbuka Daima kwa alama uliyoicha hususan kwenye Tasnia ya Habari na Michezo.



Dkt. Hassan Abbasi
**Katibu Mkuu wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo na Msemaji Mkuu wa Serikali**

UWANJA WA TAIFA SASA NI UWANJA WA BENJAMIN WILLIAM MKAPA **01**

ARIDHIO Yaleta Mapinduzi katika Upashanaji Habari **02**

BAKITA yatoa elimu kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili yanayopotoshwa **04**

**Mhariri Mkuu**
Dkt. Hassan Abbasi

**Msanifu Jarida**
Kelvin Kanje
Anitha Jonas

**Wajumbe**
Lorietha Laurence
Anitha Jonas
Shamimu Nyaki
Eliuteri Mangi
Adeldaus Kazimbaya



# UWANJA WA TAIFA SASA NI UWANJA WA BENJAMIN WILLIAM MKAPA

*Na Shamimu Nyaki – WHUSM*

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt.John Pombe Magufuli ametangaza rasmi kuwa kuanzia Julai 29, 2020 Uwanja wa Taifa uliopo Jijini Dar es Salaam umebadilishwa jina na kuitwa Uwanja wa Benjamin William Mkapa ili kumuenzi Rais huyo wa awamu ya Tatu aliyeaga dunia usiku wa kuamkia Julai 23, 2020.

Rais Magufuli ametoa tamko hilo, Julai 29, 2020 katika hafla ya kuaga mwili wa aliyekuwa rais wa Serikali ya Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa iliyofanyika katika Uwanja wa Uhuru uliopo jijini Dar es Salaam, ambapo alisema kuwa Mzee Mkapa alikuwa na mchango katika sekta ya michezo nchini hivyo taifa linapaswa kumuenzi .

"Mzee Mkapa aliujenga uwanja mkubwa wa michezo na alikua hapendi vitu viitwe kwa jina lake,lakini kwa vile sasa amelala na hawezi kuniadhibu na kwakua nimepokea ujumbe kutoka watu wengi wakiniomba nibadili jina la uwanja wa Taifa, nimekubali na sasa natamka rasmi kuwa uwanja huu uitwe Mkapa Stadium," alisema Rais Magufuli.

Aidha, Rais Magufuli alisema kuwa Mzee Mkapa ni kiongozi aliyekuwa anapenda michezo michezo na amefanya mambo mengi katika sekta hiyo,vile vile alikua ni shabiki wa timu ya Yanga ingawa hakuwahi kuonyesha hadharani hivyo watanzania wanatakiwa kumkumbuka na kutunza kumbukumbu hizo.

Halikadhalika, Rais Magufuli aliongeza kuwa Mzee Mkapa ndiye muanzilishi wa Chama cha Hakimiliki na Hakishiriki (COSOTA) ambayo ni taasisi yenye lengo la kuwasaidia wasanii kupata haki za kazi zao na katika Sekta ya Habari, alianzisha Vitengo vya Habari na Mawasiliano Serikalini.

Naye, shabiki wa mpira nchini Bw.Athuman Ugassa amepongeza uamuzi wa Rais Magufuli kubadilisha jina la Uwanja wa Taifa na kuuita Uwanja wa Mkapa kwani uwanja huo ni alama ya mchango wa Mzee Mkapa katika kuendeleza sekta ya michezo nchini.

Uwanja wa Taifa Dar es Salaam (Mkapa Stadium) ni miongoni mwa viwanja vikubwa barani Afrika ambavyo vimekidhi vigezo vyote vilivyoanishwa na Shirikisho la Soka Duniani FIFA na una uwezo wa kuingiza mashabiki takriban elfu sitini.

# ARIDHIO Yaleta Mapinduzi katika Upashanaji Habari

Na Shamimu Nyaki.

Upashanaji habari katika Dunia ya sasa umebadilika. Teknolojia ya habari na mawasiliano imewezesha taarifa kumfikia mtu kiganjani kupitia simu muda ule ule tukio linapotokea ikiwa imeabatana na picha mnato au video.

Kutokana na hilo vyombo vya habari vya zamani kama redio na televisheni navyo vimebadilika kutoka mfumo wa kurusha habari zilizopitwa na wakati hasa matukio ambayo yalikwisharushwa na mitandao ya kijamii jana yake.

Mabadiliko haya yalililazimu Shirika la Utangazaji la Taifa (TBC) kubuni mfumo mpya wa uhabarishaji ambao ulipewa jina la ARIDHIO (ikiwa na maana: habarisha, toa taarifa).

Siku za nyuma Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dkt. Harrison Mwakyembe, alizindua rasmi ARIDHIO ambayo ni ndoto yake ya siku nyingi kufuatia kauli yake aliyowahi kuitoa Bungeni jijini Dodoma kwamba siku moja TBC itakuwa zaidi ya vyombo vikubwa vya kimataifa ikiwemo CNN na BBC.

ARIDHIO ni sehemu pekee ambayo mwananchi anaweza kupata habari zenye uchambuzi wa kina kutoka kwa wachambuzi wenye weledi na uzoefu mkubwa katika masuala mbalimbali ikiwemo siasa, uchumi, teknolojia, afya, michezo na burudani.

Aidha Waziri huyo ameeleza kuwa ujio wa COSOTA katika Wizara ya Habari,Utamaduni Sanaa na Michezo utarahisisha ushirikiano na Mamlaka ya Mawasiliano nchini (TCRA) katika kulinda na kusimamia maslahi ya wasanii wa filamu na muziki pamoja na kupanua wigo wa malipo na stahili za wasanii kwa kazi zao katika majukwaa mbalimbali ya Sanaa kielektroniki.

Mhe.Waziri amesisitiza kuwa lazima COSOTA ya sasa iingie mikataba na nchi za nje ambazo vyombo vyake vya habari vimekua vikipiga muziki wa wasanii wa Tanzania bila kuwapatia gawio au kufaidika kwa namna yoyote ile.


DIRA
VSS-21PTZ


ARIDHIO



# BAKITA yatoa elimu kwa baadhi ya maneno ya Kiswahili yanayopotoshwa

Anitha Jonas – WHUSM, DODOMA

Baadhi ya watanzania wamekuwa na hulka ya kutokuwa na matumizi sahihi ya baadhi ya maneno ya lugha ya Kiswahili, hali ambayo imesababisha Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA) ikiwa ni taasisi yenye dhamana kuanza kutoa elimu sahihi yamatumizi ya maneno ya lugha hiyo.

Kaimu Katibu Mtendaji wa BAKITA Bibi. Consolata Mushi, hivi karibuni alipokuwa akizungumza kwa njia ya simu na Afisa Habari wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Wizara ya Habari, Bibi. Anitha Jonas alisema kuwa baadhi ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili wamekuwa wakifanya makosa ya matumizi ya lugha ya Kiswahili.

Aidha, Bi.Consolata alisema kuwa baadhi ya maneno yamekuwa yakitumiwa kimakosa na utumiaji huo umepelekea kuibua mgogoro wa kifikra miongoni mwa watumiaji wa lugha husika hivyo kuepukana na madhara yanayoweza kuwa makubwa ni bora kusahihisha matumizi hayo.

"Nitoe mfano ambao ulisikika siku moja kupitia chombo fulani cha habari kuwa mtaalamu wa kilimo amewaasa wakulima kutumia mbolea, utumiaji wa namna hii si tu kwamba unapotosha bali unaharibu kabisa dhana nzima ya kile kinachosemwa,"alisema Bibi.Consolata


Akitolea mfano wa maneno ambayo yanapotoshwa ni neno 'asa' kwa mujibu wa Kamusi Kuu ya Kiswahili (2015) lina maana ya "Kanya au kataza mtu kufanya jambo fulani", na kusema kuwa matumizi hayo yanaweza kupotosha na kuharibu maana ujumbe uliokusudiwa.

Vilevile, Bibi.Consolata alifafanua matumizi sahihi ya neno 'asa' kuwa linaweza kutumika kwa kuonya mfano: "Walimu wamewaasa wanafunzi kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya" au "Serikali yawaasa wazazi wanaowaachisha watoto wao shule kwa ajili ya kuwaoza.

Kwa mujibu wa BAKITA neno lingine ambalo limekuwa likipotoshwa na watumiaji wa lugha ya Kiswahili ni mrabaha, chanzo cha upotoshaji wa neno hilo ni ubadilishaji wa mpangilio wa vitamkwa vya mwisho vinavyounda neno hilo, badala ya kusema mrabaha watu husema mrahaba.

Mrabaha maana yake ni, "Malipo yanayotolewa na mchapishaji kwa mtunzi wa kitabu kwa kipindi fulani kama sehemu ya mauzo ya kitabu kinachohusika, au inaweza kuwa ni "Malipo yanayotolewa kama sehemu ya faida inayotokana na biashara fulani.

Halikadhalika, neno mrahaba halina maana yoyote katika lugha ya Kiswahili hivyo utumiaji wa neno hilo ni upotoshaji na watu wengi wamekuwa wakifanya makosa katika matumizi yake.



**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**